

Uzindushi¹ wa Lugha za Kiafrika Kinadharia: Mfano wa Lugha ya Kiswahili nchini Kenya

Mwenda Mukuthuria

Ikisiri

Kwa muda mrefu, nchini Kenya hakujawa na chombo thabiti cha ukuzaji wa istilahi za Kiswahili. Kinyume na hali ilivyo katika nchi ya Tanzania, istilahi zimeibuka na kuingia katika matumizi kutegemea mahitaji. Hata hivyo, mwaka 1998 na 1999 Rocha Chimerah alianzisha juhudzi za makusudi za kuendeleza istilahi za Kiswahili na kuziba mapengo ya kinadharia. Pia, zilenga kushughulikia mapengo ya istilahi zilizoibuliwa na utandawazi na mfumuko wa istilahi za taaluma ya kompyuta na elektroniki. Kwa hivyo, makala haya ni tathmini ya kina ya mkabala wa kiuhalisia uliozingatiwa na Chimerah katika uendelezaji wa istilahi za Kiswahili. Vigezo sita alivyovitumia kama misingi ya kuendeleza istilahi vimejengwa upya, kisha uthabiti na udhaifu wake ukachunguzwa na kuainishwa. Hatimaye, mwelekeo wa kinadharia umetolewa kwa jinsi mkabala huu unavyoweza kutumiwa katika utafiti kama "kipaimara" cha mikabala iliyoko ya utafiti wa istilahi za Kiswahili kiisimu.

1.0 Utangulizi

Karne hii imeshuhudia kupanuka kwa utafiti wa istilahi za Kiswahili kwa misingi ya kisayansi (taz. Kiingi, 1989, 1998; Mwansoko na Tumbo-Masabo, 1992; Kiango, 1996 na Were-Mwaro, 2000). Mwelekeo huu unazingatia ukweli kwamba ufanisi wa taaluma yoyote ile unahitaji utafiti. Hii ndiyo sababu Kiango (1996) anaona kwamba sayansi na teknolojia itabadili mitazamo ya kijadi kuhusu suala la istilahi. Kwa hivyo, masuala ya kiistilahi katika lugha ya Kiswahili yana manufaa makubwa, hivyo, yanahitaji kufanyiwa utafiti wa makusudi. Kwa njia hii, washiriki watakuza vipaji vya udadisi na kufungua mikabala mipy ya kuendeleza na kukuza maarifa. Kazi hii imelenga kutathmini mkabala wa utafiti wa istilahi ulioibuliwa na Chimerah (1998 na 1999) na kuhoji kufaa kwake katika utafiti wa istilahi, hasa kipindi hiki cha utandawazi na mustakabali wa Kiswahili kuwa lugha rasmi nchini Kenya.

2.0 Hali ya Istilahi za Kiswahili nchini Kenya

Hali ya istilahi nchini Kenya kwa muda mrefu imekuwa ikitia tataruki. Hii ni kwa sababu hakuna chombo wala taasisi yoyote ambayo imetwikwa jukumu la kutafiti istilahi ingawa lugha ya Kiswahili inapanuka kimatumizi kila uchao (tz. King'ei, 2000). Fauka ya haya, hakuna wafadhili wa shughuli ya utafiti wa istilahi wanaojitokeza waziwazi. Akihoji suala hili, Andala (2002) anasema kwamba kuna haja ya kufanya utafiti wa makusudi kwa sababu baadhi ya mashirika yanayodhamini utafiti yaelekeea yanaweza yasipendelee masuala ya istilahi za

¹ Istilahi hii ina maana ya kutanabahisha kwa mujibu wa Gibbe (1994)

Kiswahili. Hii ni kwa sababu miradi wanayoidhamini inalenga masilahi yao. Kwa hivyo, Andala anashauri kwamba kuna haja ya kuendeleza utafiti wa makusudi ili kuondokana na utegemezi wa mashirika ya utafiti yanayoendelea masilahi yao binafsi. Akilishadidia zaidi suala la utafiti, anahimiza kwamba utafiti wa istilahi uzingatiwe na watafiti binafsi walio na motisha na wanaojidhamini kwa sababu kwa ujumla hakuna pesa zinazoelekezwa katika utafiti wa Kiswahili (Andala, 2002: 257). Katika mkabala huu, mtafiti huyu anapiga hatua katika mwelekeo wa kutafiti istilahi za viwandani ambazo zina misingi yake katika maendeleo ya viwanda vya Jua-Kali nchini Kenya (Andala, 2000). Hatimaye, anapendekeza kwamba utafiti wa istilahi unaweza kufana pale ambapo makundi yanayojihuisha na utafiti huo yatakapokuwa yanashirikiana na vikundi ama watu binafsi wanaojibidiha kutatua tatizo hili. Maoni ya mtafiti huyu yanatudhihirishia uhalisia kuhusiana na utafiti wa istilahi nchini Kenya na Afrika Mashariki kwa ujumla. Huku tukipongeza juhudhi za TUKI (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili) ambayo kwa sasa ni TATAKI (Taasisi ya Taaluma za Kiswahili) na taasisi andamizi kule Tanzania za kuendeleza utafiti wa istilahi. Ni vyema kupendekeza kwamba pana haja ya taasisi hizi kupiga hatua ya kuwashirikisha kwa makusudi wadau wote katika eneo la Afrika Mashariki na kwingineko ili kutafiti istilahi kikamilifu. Mwito huu unadhihirishwa wazi na King'ei (2000) anaposema kwamba tangu mwaka 1964 TUKI ilipowekwa chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mchango wa Kenya kuhusiana na ukuzaji wa istilahi ulifisia kabisa. Wakati umefika ambapo asasi za utafiti zinatakiwa kuwajibika kutafuta washirika nyanjani badala ya kusubiri kuendewa na wadau.

Simala (2002) anasema kwamba kuna haja ya kutafiti istilahi za Kiswahili ili kuifanya lugha hii kwenda na wakati, kujitosheleza katika misingi ya ufaafu, umuhimu na utekelezwaji. Maneno ya msomi huyu kwa mara nyingine yanadhihirisha wasiwasi uliopo kuhusiana na istilahi za Kiswahili. Kutokana na maoni haya, ni wazi kwamba nyanjani kuna istilahi zisizofaa kutokana na watu kuijundia istilahi zao ili kukidhi mahitaji. Anashauri kwamba utafiti wa istilahi za Kiswahili uzingatie nyanja zote. Kwa mfano; sanaa, fasihi, dini, siasa, afya, mawasiliano, filamu, uchumi, elimu, sayansi, teknolojia, mazingira, maendeleo, habari, umenke na uzingiro¹. Nyanja hizi zote zina istilahi zilizoundwa na wataalamu ili kukidhi mahitaji yao. Kwa hivyo, utafiti ama miradi ikiongozwa itaibuka na istilahi nyingi pamoja na kuwashirikisha wataalamu wa nyanja hizi na asasi za utafiti wa istilahi ili kufanikisha uundaji wa istilahi za siku za usoni. Katika mwelekeo huu tunaungana na Simala kukiri kwamba hii ndiyo njia pekee ya kufanikisha utafiti wa istilahi za Kiswahili. Pamoja na nyanja zilizopendekezwa, kazi zilizotafsiriwa kwa Kiswahili zichunguzwe. Hii ni kwa sababu taaluma ya tafsiri inabuni istilahi nyingi ambazo haziwezi kuepukwa kwa urahisi (Mukuthuria, 2007). Vilevile, utafiti wowote ule unaohusisha kuathiriana kwa Kiswahili na lugha za Kiafrika uchunguzwe kwani ni chanzo kikuu cha kutudhihirishia istilahi ibuka zilizo katika matumizi (Mukuthuria, 2008). Aidha,

vyuoni wahadhirini wanaobuni istilahi kutatua matatizo ya kuwasiliana na wanafunzi wao wanahitaji kutafitiwa. Utafiti wa namna hii katika mazingira ya Kenya unahalalishwa na kauli ya King'ei (2000: 59) anaposema, "Walimu wa Kiswahili, wanafunzi na wasomi wameachiwa huria kujundia istilahi za kukidhi mahitaji yao." Kwa hivyo, mawanda haya pamoja na masuala ibuka kama demokrasia, haki za binadamu, na uraia yanatakiwa kupewa kipaumbele katika utafiti wa Kiswahili. Ifahamike kwamba maeneo haya yanahitaji utafiti wa dharura. Vilevile, vyombo vya habari visiachwe nyuma. Hivi vinazua istilahi na kuzieneza kwa haraka. Kwa hivyo, kutodhibiti mambo haya yote kumesababisha uundaji wa istilahi usio na mwongozo.

Suala la uundaji wa istilahi za Kiswahili kiuhalisia limedhihirika pia katika kazi ya Buliba (2000). Mwanalugha huyu amebainisha kwamba wataalamu mbalimbali wa isimu ya Kiswahili wanatumia istilahi tofauti, hali ambayo inasababisha kuzuka kwa utata. Anasema kwamba japo istilahi haistahili kuwa na utata, lakini hali hii inabainika katika istilahi tofauti zinazotumiwa na vyuo mbalimbali nchini Kenya. Pia, anadai kwamba tofauti hii ipo katika istilahi zinazotumiwa na wataalamu tofauti. Uchunguzi wake uligundua kwamba matumizi ya istilahi tofauti kuwakilisha dhana moja ni tatizo katika ufundishaji wa sarufi shulenii na taaluma pana ya isimu. Kwa ujumla, uchunguzi huu unabainisha kwamba usanifishaji wa istilahi zinazotumika katika isimu ya Kiswahili haujalenga mahali sahihi na hali hii inaathiri vyuo na shule za upili. Tatizo hili ni uthibitisho wa kuzua istilahi na kuzitumia bila ushirika wowote na wadau wengine katika taaluma, hali ambayo itazua vurugu isipozingatiwa kiutafiti. King'ei pia anatananabahisha kwamba tatizo hili lipo hivyo, anapendekeza suluhu ya haraka (King'ei, 2000: 61– 66).

Mwanalugha mwingine ambaye amezingatia matatizo ya uundaji istilahi nchini Kenya ni Marani (2002). Akishughulikia istilahi za kiisumu amebainisha jinsi istilahi zinazotumiwa na wataalamu katika kufunza na kuchapisha zinavyotofautiana katika mazingira ya Kenya na Tanzania. Mifano anayoitoa inazingatia ngazi mbalimbali za lugha. Kazi hii na ile ya Buliba ni kama zinajengana, kwani zote zimetoa mifano maridhawa kuhusiana na mtafaruku uliopo wa istilahi katika viwango vyote vya lugha. Tatizo wanalolibainisha ni ukosefu wa ushirikishaji wa wataalamu katika vikao vya mara kwa mara na ukosefu wa asasi thabiti za kuendeleza uundaji wa istilahi. Hali hii inachangia uundaji wa istilahi kiuhalisia katika mazingira ya Kenya. Akiikosoa hali hii King'ei (2000: 46) anasema kwamba inawafanya wasomi kuwa kwenye mashindano ya uundaji wa istilahi.

Kutokana na maoni ya wanalugha wachache ambao kazi zao zimepitawi, ni wazi kuwa:

- Hakuna taasisi ya kuelekeza uundaji wa istilahi nchini Kenya;
- Utafiti wa istilahi uko katika kiwango cha chini sana hivyo takriban mawanda yote ya taaluma hayajafanyiwa utafiti wa kutosha;

- Hakuna ushirikiano wa wataalamu wa Kiswahili na taasisi za uundaji wa istilahi;
- Hakuna mikakati ya kuunda istilahi nchini Kenya tofauti na hali ilivyo Tanzania;
- Hakuna utaratibu wa kushirikisha wataalamu mara kwa mara katika uundaji na usanifishaji wa istilahi;
- Usambazaji wa istilahi haupo laiti ungalikuwapo baadhi ya matatizo yangeepukwa; na,
- Kuna haja ya kufanya utafiti.

Mambo haya, na mengine mengi ndiyo yanayosababisha wataalamu wa Kiswahili kuhiasi kuijundi istilahi wenyewe. Matokeo ya hali hii ni kwamba:

- Kuna istilahi nyingi zinazowakilisha dhana moja,
- Kuna istilahi nyingi zisizofaa kwa kuwa hazijasanifishwa,
- Ufundishaji wa isimu na uchapishaji unaendelezwa kwa kutumia istilahi nyingi ambazo hazijasanifishwa.

3.0 Sababu Zilizomfanya Chimeraha Kuunda Istilahi

Chanzo cha uundaji wa istilahi za Kiswahili tangu awali kimetokana na upanuzi wa matumizi ya lugha hii katika nyanja mbalimbali. Shughuli za uundaji wa maneno mapya ya Kiswahili ziliongezeaka sana baada ya lugha hii kusanifishwa. Kipindi hiki kinaendana na awamu inayotajwa na Sager na Johnson (1978) inayoainisha kipindi baada ya Vita Kuu vya Pili vya Dunia kuwa lugha nyingi za ulimwengu zilihitaji msamiati wa kiufundi zaidi. Kuhusu suala hili George Mhina² anasema kwamba, “Maendeleo ya lugha huwa na maana ya ongezeko la maneno pamoja na uwezo wa lugha hiyo kukidhi haja ya mawasiliano katika nyanja nyingi zaidi ya hapo awali.” Katika mwelekeo huu, Chimeraha alishawishika kuunda istilahi kwa sababu Kiswahili kama lugha ya kimataifa kimepanuka na kuna haja ya kukidhi nyanja zinazopanuka kama vile za elektroniki na kompyuta. Zaidi ya hayo, mchango wa mtangulizi wake Nabhany (1978) ulimchochea kufanya utafiti wake. Anashauri kwamba iwapo wataalamu wangejitokeza na kuunda istilahi kwa wingi, wangefanikisha maendeleo ya istilahi za Kiswahili. Hivyo, anaouona utafiti wake kama jitihada ya kuendeleza mchango wa Nabhany. Kwa hivyo, mwelekeo wa uundaji wa istilahi uliochukuliwa na mtaalamu huyu huku akilenga mawanda ya elektroniki, kompyuta, umenke na masuala mengine ya utandawazi, ulikuwa na nia ya kuziba pengo lililo wazi katika maeneo haya ya kitaaluma. Ukweli huu unadhihirika pale ambapo Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992:12) wanaposema kuwa: “Ili mawasiliano hayo na hasa ya nyanja za kitaaluma yaweze kufanyika kwa ufanisi, hapana budi kuwepo na istilahi mwafaka za Kiswahili.”

Ifahamike kwamba japo tija ya ugunduzi wa kompyuta ilianza kuonekana katika mataifa ya kimagharibi miaka ya 1950, lakini matumizi ya kifaa hiki katika

nchi za Afrika Mashariki yalianza kukita mizizi miaka ya 1970. Kufikia miaka ya 1980, mashirika mengi na watu binafsi walikuwa na kompyuta. Hivyo, kufikia miaka ya 1990 kulizuka uhitaji wa kuelewa muundo wa kifaa hiki na shughuli kinazozitekeleza kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hali hii ndiyo iliyomchochea Chimerah kuunda istilahi nyingi za kuziba pengo hili. Vilevile, japo taaluma ya elektroniki imekuwapo kwa muda mrefu, maneno mengi yalikuwa yametoholewa tu. Hakukuwa na jitihada zozote za kuyaunda japo Nabahany alikuwa amechangia kiasi kidogo. Kwa hivyo, kutokuwapo kwa maneno asili ya kutajia vifaa vya elektroniki kulimsukuma msomi huyu kuunda istilahi.

Pamoja na mambo haya, kipindi hiki kilikuwa na ndaro nyingine ya kuzuka kwa nadharia mpya za mitazamo ya watu kuhusiana na uchumi, siasa na maendeleo ya jamii. Mkabala huu wa kiutandawazi uliozuka kutohana na shinikizo la utangamano huru, biashara huru na wepesi wa mawasiliano ya kisasa yaliyofanya ulimwengu kuonekana kama kijiji kimoja, ulihitaji istilahi za kuuelezea. Masuala ibuka pia yalikuwa nyeti katika jamii. Istilahi zilihitajika za kufafanua dhana za masuala ya kimenke ambayo yalikuwa yameanza kufundishwa katika ngazi ya vyuo vikuu. Nchini Kenya hakukuwa na chombo cha kukitegemea. Aidha, kwingineko kama Tanzania istilahi za mwelekeo huu hazikuwa zimebuniwa. Kwa hivyo, alikusudia kukidhi haja ya mawasiliano katika nyanja za kiufundi na teknolojia, pamoja na nyanja za kueneza maarifa na utaalamu wa juu vyuoni. Kwa ujumla, sababu za Chimerah zilikuwa na uhalisia kwa mujibu wa hali ya Kiswahili na uhitaji wake wa msamiati. Aidha, lengo lake liliendana na wito wa wataalamu kama Fishman (1977) ambaye alishadidia kwamba, Kenya na Afrika Mashariki zingehitaji msamiati wa kiufundi kwa dharura ili kuwezesha huduma katika nyanja nyingi za kisayansi kama vile mawasiliano, teknolojia na elimu ya juu.

3.1 Misingi ya Mkabala wa Kiuhalsia

Tasinifu ya kiujuropa illiyojitokeza katika mkabala huu ni kwamba, njia pekee ya kukuza Kiswahili kama lugha ya kimataifa ni kupanua msamiati wake (taz. pia King'ei, 2000:56). Katika kuendeleza mawazo haya, Chimerah anasema kwamba pana haja ya dharura ya kukuza Kiswahili huku misingi iliyosaidia lugha kuu za ulimwengu ikitiliwa maanani. Akilizungumzia suala hili, Chimerah (1999) anasema:

Waandishi wameibua istilahi nyingi ambazo zimenufaisha taaluma ya fasihi na mawanda mengine ya kiusomi (Tafsiri yangu).

Ama kwa hakika, hii ni njia mojawapo ya zile ambazo zinaibua istilahi ngeni katika lugha. Njia hii ni ya kawaida sana na imetumiwa na wataalamu wa lugha nyingi za ulimwengu katika kukabiliana na mapengo ya kiistilahi (taz. pia Fulass, 1971). Kwa hivyo, wataalamu hapa hawahitaji tahadhari zozote; lengo kuu kwao ni kufanikisha uhalisia wa mawasiliano. Chimerah anashikilia kwamba Kiswahili kinahitaji istilahi nyingi ambazo kwazo watumiaji wa istilahi hizo wangezitumia.

Hii ni pamoja na kuzalishwa kwa dhana nyingi kuwakilisha istilahi moja na kisha kuwaachia watumiaji kujiteulia wenyewe. Kwa hivyo, hakuona haja ya kuwa na urasimu wowote. Katika mkabala huu, mwanalugha huyu alidai kwamba mwandishi wa tamthilia ya kwanza Henry Kuria, *Nakupenda Lakini*, alilingiza mtindo mgeni kutokana na lugha yake ya mama ‘ati nini’.³ Kwa misingi hii, alidai kwamba maendeleo makubwa ya kukuza Kiswahili kwa upande wa istilahi yangeweza kufikiwa ikiwa istilahi zinazokuzwa na wataalamu binafsi zingetiliwa maanani.

Kuhusiana na utafiti wa istilahi, aliufanua mkabala ambao aliona kwamba ungeweza kutumika katika kuendeleza juhudzi za kukuza istilahi. Kwa mahitaji ya makala haya, nimeurejelea kama *mkabala wa kiuhalisia* kwa sababu unazingatia jinsi lugha inavyoweza kukua katika mazingira asilia bila kushughulikiwa ama kupewa mkondo wa kufuata.

Mkabala wa kiuhalisia unajumuisha mawazo yaliyo na uelekevu na ambayo yanaweza kutumiwa na watafiti chipukizi wa lugha ya Kiswahili katika kutafiti, kukuza, na kuendeleza istilahi za lugha ya Kiswahili. Mkabala huu unazingatia vigezo vifuatavyo ambavyo vinajibainisha katika kazi za Chimerah (1998 na 1999) kama ifuatavyo:

- (a) Kwamba, ni kweli ushahidi upo wa kutosha wa kuthibitisha kwamba dhana ngeni katika lugha yoyote ile, aghalabu huzuliwa na watu binafsi wala si majopo, na matumizi yake wanaachiwa watumiaji kujiamulia wenyewe;
- (b) Kwamba msamiati unaoundwa na wataalamu binafsi, aghalabu huchochewa na utashi wa kufanikisha mawasiliano katika muktadha maalumu;
- (c) Lengo kuu la mkabala huu wa kiuhalisia ni kutajirisha Kiswahili ili kiwe na uwezo kama lugha yoyote ile ya ulimwengu katika kuelezea mawazo, fikra, na dhana wakati wowote ule, na kupambana na mabadiliko na mageuzi ya jamii;
- (d) Unatambua kwamba juhudzi za pamoja aghalabu huwa kikwazo cha kupiga hatua ya haraka kwa sababu ya urasimu;
- (e) Kwamba kufanikiwa kwa Kiswahili siku za usoni kunategemea uwezo wa watumiaji wake wa kuelezea dhana kadhaa zinazochochewa na mapinduzi makuu ya kiteknolojia na kiutamaduni katika kipindi hiki cha historia; na,
- (f) Mkabala huu una misingi yake katika kudhibiti istilahi za Kiswahili katika nyanja zote na kuepusha lugha hii na mkasa wa kuangamia kama ilivyotabiriwa na Haney (1995) kwamba ni lugha mia sita (600) zitakazonusurika kuangamia kutoka katika jumla ya lugha elfu sita (6000) kufikia mwaka wa 2100.

3.2 Utaratibu Uliotumiwa na Chimerah Kuunda Istilahi

Kwanza, tungependa kukiri kwamba kinadharia, utaratibu wake umetimiza masharti ya msingi kuhusiana na uundaji wa istilahi. Sababu zilizomfanya kulitekeleza jukumu hili ziko wazi na mbinu alizozitumia zinadhihirika (taz. pia King'ei, 2000: 57).

Uchunguzi katika istilahi za Chimerah unabainisha kwamba amezingatia michakato iliyodhihirika kuzalisha istilahi zake. Kwa mfano, neno **tarakilishi** aliloliunda limetokana na uunganishaji wa maneno **tarakimu**, **akili** na **mashine**. Neno hili linaweza konyambulishwa, kwa mfano, kutokana nalo, vinyambulishi vifuatavyo vinaweza kupatikana: **tarakilisha**, **tarakilisisha** na kadhalika. Mionganoni mwa mbinu nyingine za uundaji wa maneno zinazodhihirika katika istilahi zilizoundwa na Chimerah ni ile ya ukopaji na kuasilisha maneno. Kwa mfano, istilahi zifuatazo zinatokana na neno la mkopo ambalo limeasilishwa:

kukoda	-	<i>to code</i>
kukoudua	-	<i>to decode</i>
kukodesha	-	<i>to codify</i>
kukodeshwa	-	<i>to be codified</i>
kukodewa	-	<i>to be coded for</i>
kukodwa	-	<i>to be coded</i>

Katika mifano hii, istilahi zilizokopwa zimetoholewa na konyambuliwa kwa kutumia mnyambuliko sarufi na mnyambuliko geuzi ili kukidhi mahitaji ya istilahi katika lugha ya Kiswahili. Vilevile, ametumia mbinu ya tafsiri, kwa mfano:

kifaororo	-	<i>software</i>
kifaanyumu	-	<i>hardware</i>
vuna data	-	<i>harvest data</i>

Amejitahidi kuunda istilahi zilizo na mtiririko na utimilifu wa kuridhisha. Mathalani, ameepuka mtindo wa kuunda istilahi mojamoja ambao unasababisha uundaji wa istilahi zisizo na mtiririko; kwa mfano:

menke	-	<i>gender</i>
menke ya kisarufi	-	<i>grammatical gender</i>
nyazogande za kimenke	-	<i>gender stereotype</i>
wazogande	-	<i>stereotype</i>
utambulisho menke	-	<i>gender identity</i>
ukitishaji menke	-	<i>gender positioning</i>

Mifano hii ni uthibitisho kwamba alizingatia kuunda istilahi nyingi kadiri iwezekanavyo kuziba pengo la dhana mahususi katika uwanja fulani. Kwa njia hii, ni wazi kwamba anatambua dhana zinazowakilishwa na istilahi kwa kawaida huwa hazikai pwekepweke.

Mtaalamu huyu alizingatia pia utafiti wakati wa kuunda istilahi zake. Baadhi ya istilahi alizoziunda ziliwasilishwa katika kazi zake maarufu za miaka ya 1998 na 1999. Uundaji wake ulikuwa na utaratibu maalumu wa dhana mpya na istilahi zake. Istilahi alizoziunda zilienezwa kupitia kazi hizi za kiutafiti na nyingine alikabidhi mashirika ya utangazaji nchini Kenya na nchi za nje ambayo yalikuwa yanazihitaji kwa ajili ya kufanikisha mawasiliano katika vyombo vya habari. Kwa hivyo, ni wazi kwamba alizingatia baadhi ya misingi iliyokuwa imependekezwa na Sager na Johnson (1978) na baadaye Felber (1980) kama vile:

- Kuanzia uundaji wa istilahi na dhana;
- Kuelezea dhana kwa uwazi na ukamilifu;
- Kuchukulia uhusiano wa dhana kama msingi wa kuunda istilahi;
- Istilahi zilikopwa anazichukua kama zilivyo katika umbo lake la asili kwa kufanya marekebisho machache kulingana na matamshi ya lugha ya Kiswahili;
- Kuzingatia sarufi ya lugha ya Kiswahili;
- Kupatia istilahi muundo unaoeleweka kulingana na mofolojia ya kawaida ya lugha ya Kiswahili; na,
- Kuunda istilahi ambayo itakubali kuunda nyingine kwa njia ya mnyambuliko.

Utaratibu huu unabainisha uzingativu wa misingi ya sayansi katika uundaji wa istilahi. Pengine kilichobakia ni kuelekeza utafiti wa kukamilisha shughuli hii kwa kuchunguza kufaa kwa istilahi hizi kwa misingi ya usayansi (taz. Were-Mwaro, 2000).

4.0 Tahakiki ya Mkabala wa Kiuhalsia na Hali ya Lugha ya Kiswahili

Vigezo vya mkabala huu vikichunguzwa kwa jicho pevu vina nguvu na udhaifu wake. Tukiangalia kigezo cha kwanza, watu binafsi wamechangia kwa kiwango kikubwa kuzua baadhi ya istilahi zinazotumika katika Kiswahili Sanifu (taz. Nabhan, 1978; Njogu na Chimerah, 1999; Chimerah, 1998 na 1999; Were, 2000 na Njogu, 2002). Kwa hivyo, kinatuelekeza kutahadharisha wasomi na wapenzi wa Kiswahili walio na mtindo huu kumakinika wanapokumbwa na hali ambayo ingeweza kuwasababishia kuzua istilahi ya/za kutumia. Katika kipindi hiki cha utandawazi na mawasiliano pevu, hakuna haja ya mtaalamu kujifunga na kubuni istilahi akiwa pekee. Hii ni kwa sababu njia za mawasiliano zinaweza kusaidia kupata maoni kutoka asasi za uundaji wa istilahi au wataalamu mahususi wa lugha husika kutoka pembe zote za dunia kwa kutumia barua pepe au tovuti (mtando). Kwa hivyo, ni vema kuepuka mtindo huu kwa sababu unaweza kuzua vurugu katika istilahi za Kiswahili (linganisha na Massamba, 1989). Hata hivyo, kutokana na kigezo hiki, tunaweza kusema kwamba kina manufaa katika utafiti wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu ikiwa tutapanua istilahi za Kiswahili zilizopo, basi

itatubidi sote tuelekeze juhudini za utafiti kwa wataalamu wote wa Kiswahili, hasa wa Afrika ya Mashariki na kuchunguza istilahi wanazozitumia kwa ajili ya kusanifishwa. Kwa kufanya hivi, tutaimarisha ushirikiano wa uundaji wa istilahi na kuepuka mtindo huu ambao umepitwa na wakati. Ifahamike kwamba mtindo huu hauwezi kufa kabisa. Jambo la muhimu ni kudhibiti kiwango cha uzalishaji wa istilahi kwa njia hii kupitia utafiti. Aidha, uundaji wa dhana ngeni uzingatiwe pale ambapo mbinu nyingine za uundaji wa istilahi zimeshindwa. Ikiwa kwa mfano, watumiaji na wataalamu wa lugha ya Kiswahili wataachiwa kujamulia istilahi wenyewe, basi kuna hatari kubwa ya kuwa na ‘viswahili’ mbalimbali na wataalamu hawataelewana. Vilevile, uchapishaji wa lugha ya Kiswahili utakuwa umedumazwa hali ambayo itakwaza maendeleo ya lugha ya Kiswahili katika kipindi hiki cha utandawazi.

Japo majopo hayawezi kuzua dhana ngeni lakini ni busara kuyatumia kuhakiki dhana hizo ngeni, kwa hivyo, yasipuuze. Cha muhimu ni kuwa na majopo tekelezi ambayo yanakutana katika kipindi mahususi. Kwa kufanya hivi, watumiaji wa lugha ya Kiswahili wataweza kuwasiliana nao kwa urahisi. Aidha, ni busara kutambua kwamba majukumu ya majopo kama haya ni makubwa mno. Kwa hivyo, ningependekeza kwamba ikiwa majopo yatatumika, basi kila nchi iwe na jopo. Aidha, majopo hayo yawe yana uwezo wa kuwasiliana.

Dhana ngeni na msamiati unaoundwa na watu binafsi unaochochewa na utashi wa mawasiliano ni kigezo cha pili cha mkabala wa kiuhalisia ambacho kina ukweli usiopingika. Kina misingi ya usayansi kwa kuwa utashi wa mawasiliano ni sharti uwepo kabla ya kuunda istilahi. Kwani mawasiliano kwa kiwango kikubwa yanachochea kuathiriana kwa lugha (Mukuthuria, 2004). Mawasiliano ya maandishi na ya mazungumzo ni vyanzo vikubwa vyta dhana ngeni na vichocheo vikuu kwa wataalamu wanaobuni istilahi. Mathalani, mazingira ya darasani yamechochea walimu kuibuka na istilahi za kufanikisha uwasilishaji wa masomo yao kwa wanafunzi, hasa somo la tafsiri (Mukuthuria, 2007). Akitoa mfano ulio na mwelekeo huu, Chimerah (1999) anasema istilahi za Kimani Njogu **ubwege** ‘absurd’, **usemezo** ‘dialogism’, na **undenguzi** ‘deconstruction’ ni miongoni mwa istilahi zilizoundwa na mtu binafsi katika mazingira ya darasani na zikaingia katika mkondo wa matumizi (taz. Njogu na Chimerah, 1999). Pia, harakati za kuwasilisha kazi za kiutafiti zimechangia wasomi kuibua istilahi mbalimbali za kutumiwa katika ripoti zao (Buliba, 2000; Marani, 2002; Mukuthuria, 2009). Kwa hivyo, ni vema utafiti wa istilahi uelekezwe katika mazingira ya darasani na kwa upande wa kazi mbalimbali za utafiti wa Kiswahili na ule uliofanywa kwa kutumia lugha ya Kiswahili ili kujenga kanzi ya istilahi za kusanifishwa. Kwa kufanya hivi, Kiswahili kitaneemeka na jitihada za walimu, wanafunzi na wataalamu (King’ei, 2000: 59). Kwa ujumla, kigezo hiki kinaweza kutumiwa na wataalamu wa Kiswahili kuelekeza miradi na tasinifu za wanafunzi.

Japo kigezo cha tatu kina manufaa kwa lugha yoyote ile, lakini kina upotoshaji mkubwa. Iteleweke kwamba zamani lugha kuu za ulimwengu kama

Kiingereza zilipokuwa zikienea kwa haraka, teknolojia ya mawasiliano ilikuwa katika kiwango cha chini ikilinganishwa na hali ilivyo sasa. Kwa hivyo, japo tunataka kutajirisha lugha ya Kiswahili hatuwezi kusifu njia za mikato ili tuweze kutosheleza mawazo, fikra na dhana. Kipindi hiki, taasisi kuu za uchunguzi wa Kiswahili zina uwezo wa kutimiza matilaba haya kwa njia za kisasa zisizo za kiholela zinazozingatia misingi ya sayansi (taz. Kiango, 1996). Kwa hivyo, hapana haja ya wataalamu wa Kiswahili kutaharuki na kujiundia istilahi zinazokinzana na za Taasisi za Uchunguzi wa Kiswahili. Mfano wa istilahi iliyoundwa kiholela siku za karibuni na ambayo imesikika ikitumika katika vyombo vya habari katika mazingira ya Kenya ni *gatuvi* kwa maana ya **kaunti**. Istilahi *gatuvi* imetokana na neno ugatuvi. Istilahi hii ilibuniwa huku istilahi kaunti ikiwa inatumika kwa mapana na mrefu nchini Kenya baada ya kupitishwa kwa katiba mpya iliyosababisha kuhalalishwa kwa utawala uliozingatia muundo wa majimbo nchini Kenya. Maoni yetu hapa si kwamba neno *gatuvi* halivezi kutumika. Tatizo ni kwamba: je, neno *gatuvi* litatumwa na nani mbele ya neno kaunti ambalo lina mashiko na ukubalifi zaidi? Kilicho na umuhimu hasa istilahi zinapoundwa ni kwamba ieeweke ukubalifi ni kigezo kimojawapo cha vigezo vya usayansi. Pia, tunashauri kwamba istilahi za mkopo ama zilizotoholewa zisionekane kana kwamba hazina nafasi katika uendelezaji wa istilahi za Kiswahili. Kwa mfano lugha ya Kiingereza, ambayo ni lugha ya ulimwengu ingejibana kwa kutokubali msamiati wa lugha nyingine za ulimwengu, leo ingekuwa wapi? Vilevile, tusipokopa msamiati wa kisayansi ulio na misingi yake katika tamaduni mbalimbali za ulimwengu, watumizi wa Kiswahili watatoo istilahi faafu wapi za kuwakilisha dhana hizo? Haya ni mambo ya kimsingi ambayo kila mpenzi wa Kiswahili anapaswa kuelewa. Kwa kuwa muundo wa Kiswahili wa kisarufi utabakia uleule ni vyema wataalamu wasipandwe na jazba za kufikiri kwamba Kiswahili kitapoteza uasili wake. Fikra kama hizo zina ‘umapokeo’ usiopeleka Kiswahili mahala popote kipindi hiki cha utandawazi.

Kigezo cha nne kwamba juhudzi za pamoja ni kikwazo kina mashiko tu pale ambapo tutaona kama mwiko kuwashirikisha watafiti binafsi kuendeleza utafiti wa istilahi. Hata hivyo, pale ambapo uamuzi wa dhana ngeni zinazoibuka kutokana na utafiti wa kibinafsi/kikundi unahitajika, juhudzi za pamoja zina manufaa makuu katika kipindi hiki kuliko hapo awali. Hii ni kwa sababu teknolojia ya mawasiliano imeimarika kupitia tovuti ama simu, pana uwezekano wa kuwa na uamuzi wa haraka ikilinganishwa na hapo awali.

Kigezo cha tano kina umuhimu mkubwa katika lugha ya Kiswahili. Iwapo lugha hii itafanikiwa katika mawasiliano, basi utafiti wa kiistilahi hauna budi kuelekezwa katika nyanja mbalimbali za kiteknolojia, kiutamaduni, kisiasa na nyinginezo. Haya yatawezekana tu pale ambapo wataalamu wataelekeza juhudzi za makusudi za kuchunguza nyanja hizi bila kusubiri. Kwa kufanya hivi, matatizo ya istilahi yatakabiliwa. Katika mwelekeo huu, juhudzi ambazo zilizalisha *Kamusi ya Biashara*, na *Kamusi ya Sheria* na nyingine zilizochapishwa na Taasisi ya

Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, zinastahili kuendelezwa. Hii ni kwa sababu ni kupertia utafiti wa namna hii, istilahi za mawanda mbalimbali ya kielimu zitapatikana kwa urahisi.

Hatimaye, hapana haja ya kuonea Kiswahili hofu kwamba kinaweza kuangamia nyakati hizi. Kwa hakika, juhudini zilizokwisha kutekelezwa kuhifadhi lugha hii ni nyingi. Wataalamu na wapenzi wa Kiswahili hawana haja ya kutaharuki kuunda msamiati kiholela kuepusha mkasa wa Kiswahili kuangamia. Utaratibu wa shughuli hii ndio unaotakikana ili kukipatia Kiswahili hadhi inayostahili kupambana na lugha nyingine kuu za ulimwengu.

5.0 Hitimisho na Mapendekezo

5.1 Hitimisho

Hatua za kuhoji mkabala wa Chimerah zinadhihirisha kwamba una nguvu na udhaifu. Licha ya udhaifu huu, ni wazi kwamba nguvu ama uthabiti wake ukiielekezwa ipasavyo kitaalamu unaweza kutumika kuendeleza juhudini za uchunguzi katika istilahi za Kiswahili. Kwa njia hii, istilahi ambazo zinatumwiwa na wataalamu mbalimbali katika kuwasilisha masomo ama matokeo ya utafiti wa nyanjani zinaweza kuorodheshwa. Kutokana na kanzi hii, majopo ya wataalamu na asasi za usanifishaji wa istilahi yanaweza kupata data ya kurejelea wakati wa kusanifisha istilahi za mawanda mbalimbali. Kwa kufanya hivi, Kiswahili kitaweza kuelezea dhana ngeni, fikra, na mawazo ambayo bila kupata maelezo yanaweza kusababisha lugha ya Kiswahili kuingiza athari za lugha ya kigeni kwa wingi.

Japo mkabala huu unadhalilisha juhudini za pamoja, lakini ukweli uliopo ni kwamba, mtu binafsi hawesi kufanikisha uundaji wa istilahi bila kuwatambua wenzake. Kinyume na mkabala wake, Chimerah (1999) anatambua juhudini za pamoja anaposema kwamba:

Natambua juhudini ambazo zimefanywa na wataalamu wa leksikografia, hasa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao wamefanya kazi za kupigilia mfano, hasa katika uwanja wa isimu.

Kutokana na kauli hii, inaweza kuamuliwa kwamba mkabala unaofaa ni ule unaoshirikisha majopo na watu binafsi katika utafiti. Hata hivyo, usanifishaji uzingatie juhudini za pamoja na maamuzi ya matumizi pia yasiachiwe watu binafsi. Njia za utafiti na majopo ya wataalamu yatumiwe kutekeleza shughuli hii. Ni wazi kwamba Kenya inahitaji kuchukua hatua za dharura kuhusiana na jitihada za kukuza na kuelekeza msamiati na istilahi katika mawanda mbalimbali ikiwamo miktadha mahususi ya kijamii. Kwa mfano, juhudini za TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, za kuunga mkono matumizi bora ya msamiati zinafaa kuigwa. Tukio la 18/8/2004, ambapo TUKI ilishirikiana na Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA) kuhimiza wanamuziki wa kizazi kipyaa kutunga ushairi na

kughani nyimbo zinazozingatia miundo fasaha na Kiswahili Sanifu, katika nyimbo zao za kufokafoka, ni hatua ya kutia moyo katika mwelekeo huu ikizingatiwa kwamba pamoja na washiriki wengine, Mkurugenzi wa TUKI, wakati huo Prof. Mulokozi, alishiriki na mwenyekiti wa waamuzi siku hiyo, Prof. Senkoro kutoka Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

5.2 Mapendekezo

Kutokana na hoja ambazo zimejadiliwa katika makala haya, ili kuimarisha uundaji na ukuzaji wa istilahi za Kiswahili, inapendekezwa kwamba:

- Kamati za kuunda istilahi za Kiswahili ziwe za kitaifa. Bila kuwa na kamati za kitaifa, msamiati wa kukurupuka unaoundwa na watu binafsi utaendelea; hivyo, kuzusha vurugu katika lugha ya Kiswahili. Mwelekeo huu utakishushia Kiswahili hadhi hasa kipindi hiki ikizingatiwa kwamba kwa sasa kimekubalika kama lugha rasmi ya nchi mbili za Afrika Mashariki, Kenya na Uganda.
- Pana haja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuharakisha mchakato wa kuweka amara imara za shirikisho ili chombo cha kukuza istilahi kilicho na kamati katika nchi zote zilizoundwa jumuiya hii kianzishwe. Bila shaka chombo hiki kitakuwa na uwezo mkubwa wa kupambana na matatizo ya kuunda istilahi katika nchi za Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda na Burundi.
- Taasisi za uchunguzi zote za shirikisho, idara za Kiswahili za vyuo, na mabaraza ya kitaifa ya nchi zinazotumia Kiswahili yashirikiane katika uundaji wa istilahi. Kwa jinsi hii, wataalamu watashughulishwa kikamilifu na hakutakuwa na haja ya kuzua istilahi kiholela.
- Inapendekezwa kwamba miongozo iliyopo kuhusiana na uundaji wa istilahi ienezwe kwa wataalamu na vyuo. Kazi ya Were-Mwaro (2000) imetoa suluhu kuhusiana na tatizo hili. Iwapo mwongozo kamia huu na mingine itatiliwa maanani na wataalamu wa vyuo, bila shaka istilahi za kufana zitaundwa.
- Wataalamu wa Kiswahili hawana budi kushirikiana katika uundaji wa istilahi. Pale ambapo istilahi fulani inafaa na kuafiki dhana, isitupwe kwa sababu imeundwa na mtaalamu fulani. Aidha, istilahi zisionekane kama za watu binafsi au vyuo mahususi. Hali ilivyo ni kwamba wataalamu hawashirikiani kikamilifu katika uundaji wa istilahi. Kwa hivyo, inapendekezwa kwamba ili kudumisha hadhi ya Kiswahili, jambo hili sharti litiliwe maanani ili kusiwe na tofauti ya Kiswahili sanifu kinachotumika Rwanda, Burundi, Kongo na ulimwenguni kwa ujumla.
- Pana haja ya mashirika yatakayoundwa na kuwezeshwa kuendeleza shughuli za kieneo na za kitaifa za istilahi kushirikiana na watu binafsi/vikundi vya watu. Asasi hizi pia ziondoe urasimu mwingu ili

kuyutia na kushirikisha wadau wengi. Aidha, zisingoje watu kuziendea; badala yake ziwaendee. Mtindo wa kizamani ukomeshwe kwa sababu lengo la asasi hizi ni utafiti na utafiti huu hauwezi kukamilika wakiwa ‘wamekanyaga mazulia’ bila kwenda nyanjani.

- Ni wazi kwamba kuna istilahi nyingi za kutafsiri na zilizobuniwa na wataalamu wakati wa utafiti. Hizi zote zinahitaji kutafitiwa pamoja na zile ambazo zimeingia katika mkondo wa matumizi. Huu ndio utafiti wa makusudi ambao unaweza kuleta tija kuhusiana na masuala ya kiistilahi. Istilahi hizi zifanyiwe majaribio ya kisayansi na kuenezwa ipasavyo.
- Pana haja ya dharura ya kufanya utafiti wa pamoja (taz. pia Andala, 2002).

Hali hii itapunguza gharama. Aidha, makongamano ya kila mwaka yanaweza kuandaliwa ambapo wataalamu wanaweza kujadili istilahi za Kiswahili zinazotumika katika mazingira na mawanda mbalimbali. Baadaye, wataalamu wa lugha walio na uzoefu wa uundaji istilahi wanaweza kutwikwa jukumu la kukagua ufaafu wa istilahi hizo. Kwa kushirikiana na vyuo na taasisi za uchunguzi, wanaweza kuchapisha toleo la istilahi mwafaka ambalo likisambazwa vyema linaweza kuwafaa wasomi. Inapendekewa kwamba tovuti ya CHAKAMA (Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki) ni njia mwafaka ya kufanya usambazaji huu. Pamoja na kufanya hivi, istilahi zinazoibuka zinaweza kutumiwa kudurusu kamusi za mawanda mbalimbali; hivyo, kujenga kanzi ya msamiati wa Kiswahili. Hatimaye, msamiati huu unaweza kutumiwa kuunda kamusi kubwa itakayoingizwa katika tovuti iliyo na maneno mengi kwa ajili ya kueneza istilahi mpya zitakazoundwa. Tovuti ya CHAKAMA inaweza kutumiwa kusambaza kamusi hii kwa ajili ya kurejelewa na watumiaji wa Kiswahili popote duniani. Njia hii itapunguza gharama ya uchapishaji wa kamusi kubwa ambazo zinasemekana kwamba katika mazingira ya Afrika Mashariki haziwezi kupata wanunuzi kwa sababu ya umaskini na viwango dhalili nya elimu.

- Utafiti kuhusiana na istilahi uandamanishwe na taaluma ibuka na pendwa kama vile, uraia, demokrasia, haki za binadamu na kadhalika (Njogu, 2002; Mukuthuria, 2004). Kwa kufanya hivi, istilahi zitakazoibuka zitakuwa mujarabu kwa nyanja husika na zitatoa suluhu ya moja kwa moja.
 - Istilahi nyingi ambazo zimeundwa na wataalamu binafsi zichunguzwe iwapo zinatimiza vigezo nya kufaa na kusambazwa ili ziwe suluhu kwa matatizo yaliyopo ya istilahi.
-

Ufafanuzi

1. Tazama Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992: V) sehemu ya dibaji ya *Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili*.
2. Kwa mujibu wa Chimerah (1998) kiulizo ‘ati nini?’ kimetokana na muundo wa Kikikuyu *ati ki?* Anaelezea kwamba ‘ati’ ya Kiswahili ikitumika katika muundo kama huu, kwa mfano, “Ati fulani amekufa?” Maana yake huwa ‘Ni kweli fulani amekufa?’ Pia, “Ati ataka kunioa?” ni usemi unaotumiwa kukejeli (uk. 42).
3. Mkabala huu unapingwa na wataalamu wa lugha kama King’ei (2000: 66) na ni katika mwelekeo huu ambapo makala haya yameazimia kuutathmini na kuutafutia mahala pake katika utafiti wa istilahi.

MAREJEO

- Andala, M. (2002). "Kiswahili Research Funding." Katika: K. Inyani Simala (Mh.). *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press (kur. 254 – 257).
- Andala, M. (2000). "Mawasiliano Viwandani: Chaguo Lipi?" Makala Iliyowasilishwa katika Kongamano la Chakita Mombasa, Oktoba 2000.
- Buliba, A. (2000). "Utata katika Istilahi za Isimu ya Kiswahili." Katika: Kimani Njogu na wenzake (Wah.). *Kiswahili Karne ya Ishirini na Moja*. Cape Town: Centre for Advanced Studies of African Society (kur. 11 – 24)
- Chimerah, R. (1998). *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Chimerah, R. M. (1999). Kiswahili Through Ages: The Question of Lexicon. [Unpublished paper] Egerton University.
- Chuwa, A. R na Tumbo-Masabo, Z. N. (1999). *Kamusi ya Biashara na Uchumi*. Dar es Salaam: TUKI.
- Felber, H. (1980). "International Standardization of Terminology and Methodological Aspects." In: *International Journal of The Sociology of Language* (23, pp. 65 – 79).
- Fishman, J.A. (1977). "Comparative Study of Language Planning Introducing a Survey." In: J. Rubin et al (ed.) (pp. 31 – 39).
- Fulass, H. (1971). "Problems of Terminology." In: Whiteley, W.H. (ed.); *Language and Social Change*. London: O.U.P., International African Institute (pp. 309 -317).
- Gibbe, A. G. 1994. *Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia*. Tasnifu ya Uzamifu [Isiyochapishwa] Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.
- Haney, Daniel (1995, February 28). Linguistic Crisis Looms as Native Tongue Die. *Daily Nation Newspaper*. Nairobi Kenya.
- Kiango, J.G. (1996) "Ukuzaji wa Kiswahili Karne ya 21." Katika: Y.M. Kihore na A.R. Chuwa (Wah.): *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja*. Dar es Salaam, TUKIKIINGI, K. B. 1989. *A Systematic Approach to the Problem of the Expressional Modernization in the formal and Natural Sciences: The Case of Luganda*. [Unpublished] PhD. Thesis, University of Bielefeld.
- Kiingi, K. B. (1998). *A Theory of Scientific Terminology*. D. Litt. Thesis, Kenyatta University Kiingi, K. B.
- King'ei, K. (2000). "Kiswahili Technical Terminology: Problems of Usage and Development in Kenya." In: Y.M. Kihore (ed.). *Kiswahili*. Dar es Salaam, TUKI (pp. 55-67) .
- Luganda, M. (2002). "Mikakati ya Kushirikisha Kenya katika Uundaji na Usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili." Katika: K. Inyani Simala (Mh.). *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press (kur. 121 -127).

- Marani, J. (2002). "Usanifishaji wa Istilahi za Utafiti wa Isimu-Muundo wa Kiswahili." Katika: K. Inyani Simala (Mh.). *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press (uk. 108 – 120).
- Massamba, D.P.B. (1989). "An Assessment of the Development and Modernisation of the Kiswahili Language in Tanzania." In: Florian, C. (ed.). *Language Adaptation*. New York: C.U.P. (pp. 60-78).
- Mlacha, S. A. K. (1999). *Kamusi ya Sheria*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, TUKI.
- Mukuthuria, M. (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunzi wa Tigania, Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu [Isiyochapishwa] Chuo Kikuucha Egerton.
- Mukuthuria, M. (2007). "Mchango wa Tafsiri katika Tanzu za Kitaaluma za Kiswahili." Katika: *Kiswahili na Elimu nchini Kenya*. Kimani Njogu (ed.). Nairobi, Twaweza Communications (kur. 119 – 134).
- Mukuthuria, M. (2009). "Uhakiki wa Mtafaruku wa Istilahi za Kiisimu na Nafasi ya Usanifishaji katika Maendeleo ya Kiswahili." Katika M. M. Mulokozi na G. Mrikaria (Wah.) *Mulika* Na. 28, TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Uk. 48-61).
- Mukuthuria, M. (2008). "Uchunguzi wa Athari kama Nyenzo ya kufunza Lugha." Katika *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Nathan Oyori Ogechi na wenzake (Wah.). Eldoret, Moi University Press (uk. 375 – 386).
- Mwansoko, H. J. M. na Tumbo-Masabo, Z.N.Z (1992). *Kiongozi cha Uundai wa Istilahi za Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, TUKI.
- Nabhany, S. A. (1978). Kadi ya Kiswahili. Mswada ambao haujachapishwa.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. (2002). "Kiswahili, Utawala, na Mageuzi ya Katiba." Katika: K. Inyani Simala (Mh.). *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press (kur. 238 – 253).
- Sager, J. C. and Johnson, R. L. (1978). "Terminology: The State of the Art." In: *Der Sprachmitter* 16, 4: 82 – 95; AILA Bulletin (22: 1 – 11).
- Simala, K.I. (2002). "Gharama za Utafiti wa Kiswahili." Katika: K. Inyani Simala (Mh.). *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press (kur. 258 – 267).
- TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Were-Mwaro, A. G. (2000). *Usayansi wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamifu [Isiyochapishwa] Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.